HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA PWANI, MHESHIMIWA ENG. EVARIST NDIKILO, WAKATI WA UFUNGUZI WA MKUTANO MAALUMU WA BARAZA LA BIASHARA MKOA WA PWANI TAREHE 24 OKTOBA 2020

- ***Ndugu Katibu Tawala Mkoa, Dkt Delphine Magere,***
- ***Katibu Mtendaji Baraza la Biashara la Taifa (TNBC) - Dkt. Godwin George Wanga,***
- ***Rais TCCIA Taifa, Joseph Njile,***
- ***Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Pwani, Joseph Njile,***
- ***Mkurugenzi Mkuu Shirikisho la Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) Veneranda),***
- ***Mwenyekiti Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Pwani, Abdallah Ndauka,***
- ***Wawekezaji wa Viwanda wote (Vikubwa kati na Vidogo)***
- ***Wafanyabiashara wote (Mama lishe, Machinga, Bodaboda, wavuvi, wafugaji, Wakulima, wasafirishaji, wamiliki wa Shule Binafsi na wengine Mliopo hapa),***
- ***Wakuu wa Taasisi za Serikali,***
- ***Wakuu wa Taasisi za Fedha (Mabenki yetu NMB, CRDB, NBC),***
- ***Wadau wa Sekta mbalimbali***
- ***Watendaji wote wa Serikali ngazi za Mkoa, Wilaya na Halmashauri,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema aliyetuwezesha kukutana mahali hapa siku ya leo.

Pili Nawashukuru sana Sekta Binafsi Mkoa wa Pwani kwa Ushirikiano Mkubwa Mliotupa Viongozi wa Serikali kuanzia ngazi ya kitongoji, Kijiji, Halmashauri, Wilaya na Mkoa kwa kipindi cha Miaka mitano 2015-2020.

Namshukuru Katibu Tawala Mkoa na Baraza la Taifa la Biashara kwa kuandaa kikao hiki muhimu cha kutathimini na Kupokea taarifa ya miaka mitano (5) ya Mafanikio ya Sekta Binafsi Mkoani Pwani na mapendekezo yao kwa Serikali. **Hongereni sana.**

Ndugu Washiriki;

Kama nilivyosema tumeona tukutane katika kipindi hiki kupokea taarifa ya mafanikio yenu na mapendekezo kwa Serikali inayomaliza muda wake. Kama mnavyofahamu Serikali iliyoko madarakani ilinadi ilani yake ya Uchaguzi kwa Mwaka 2015 na Wananchi wakiwemo ninyi mliikubali na kuipa ridhaa ya kuongoza kwa miaka mitano. Ukurasa wa 56-61 Ibara ya 44-49 katika Ilani ya Uchaguzi CCM ya Mwaka 2020 inazungumzia Sekta ya Viwanda na Biashara. Na mafanikio yaliyopatikana kipindi cha mwaka 2015-2020 na matarajio yake itakapopewa dhamana na wananchi mwaka 2020 -2025.

Ndugu Washiriki;

Naomba niwakumbushe kwa uchache mafanikio ya Mkoa wetu kwa kipindi cha miaka mitano (2015-2020) wakati wa utekelezaji wa Ilani ya CCM, mnayafahamu ila naomba niyaainishe;

1. Kuboresha mazingira ya kufanyia biashara katika Mkoa wetu, ambapo tumeweza Kufanya vikao vya Mabaraza ya Biashara ngazi ya Wilaya na Mkoa, ambapo Sekta binafsi na Umma

hukutana kujadiliana nini kifanyike katika kutatua changamoto mbalimbali.

2. Tumefanikiwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vipya 936 na kufanya Mkoa wetu kuwa na viwanda 1,236 (Vikubwa 68, Kati 112, Vidogo 168, na Vidogo sana 888). Mwaka 2015 tulikuwa na Viwanda 300.
3. Tumeanzisha madawati ya Uwekezaji (Investment Desk) ngazi ya Wilaya na Mkoa ili kuhudumia kwa ukaribu wawekezaji wetu.

4. Tumefanya ziara za mara kwa mara kukagua miradi ya Sekta binafsi kujua maendeleo yao, changamoto wanazokumbana nazo na kuzipatia ufumbuzi,

5. Tumeanzisha urafiki na Nchi ya China Jimbo la Fujian mwaka 2018 ambapo walikuwa tayari kuelekeza wafanyabiashara wao kuwekeza kwenye Mkoa wetu wa Pwani.

6. Tumefanya ziara za kikazi mwaka 2017 kwenye Majimbo ya Shanghai, Guangdong, Anhui na Beijing Nchini China kuuza Fursa za Uwekezaji zilizopo Mkoani Pwani.

7. Tuliandaa na Kufanya Maonesho makubwa ya Viwanda na Biashara kwa miaka miwili (2) (2018 na 2019) ili kutangaza bidhaa na kuufahamisha Umma kuhusu uwepo wa Viwanda vya aina mbalimbali katika Mkoa wa Pwani vikiwemo vile vinavyotumia malighafi za hapa nchini.

8. Tumeandaa Mwongozo wa Uwekezaji wa Mkoa wa Pwani mwaka 2019 (Pwani Region Investment Guide) ulioainisha Fursa zote za

Uwekezaji zilizopo kwenye Halmashauri zetu zote za Mkoa wa Pwani na kuzitangaza kupitia Tovuti ya Mkoa, Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Diaspora, Ziara za viongozi na Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Kikanda.

9. Tumewasaidia wawekezaji kuwasiliana na Taasisi wezeshi za kitaifa ili kutatua changamoto wanazokumbana nazo, NEMC, TBS, DAWASA, TIC, TRA, OSHA, WMA, BRELA, TANESCO n.k.

10. Tumetenga Maeneo kwa ajili ya Ujenzi wa Viwanda ambapo jumla ya hekta 53,651.94 zimetengwa kwenye Halmashauri zote 9 za Mkoa wa Pwani.

11. Kufuta baadhi ya Mashamba pori na maeneo ambayo hayajaendelezwa yarejeshwe Serikalini ili kupangiwa matumizi upya ikiwemo ujenzi wa viwanda. Miongoni mwa mashamba yaliyorudishwa ni pamoja na linalomilikiwa na Kampuni ya UFC ekari 5,957 lililopo Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha.

12. Tumefanikiwa na kuhakikisha kwamba wananchi, viongozi na watendaji tunaongea lugha moja katika kuvutia uwekezaji ikiwemo kuondoa urasimu usio wa lazima kwa watendaji na taasisi wezeshi, mfano TANESCO, DAWASA, TRA, Uhamiaji, na Zimamoto, NEMC, TBS, n.k.

13. Tumehamasisha matumizi ya Gesi asilia ambapo hadi sasa Viwanda vikubwa viwili (Goodwill Ceramics (T) Ltd cha vigae kilichopo Mkuranga kinachotumia gesi kutoka Gate valve Na. 12 iliyopo Mkiu, na Kiwanda cha Lodhia Group cha Chuma kilichopo Mkuranga kinatumia gesi kutoka Gate valve Na. 13 iliyopo Mbezi.

Aidha, Mkoa una tawi lingine Gate valve Na. 11 iliyopo Bungu Kibiti. Mkoa mpaka sasa umewaomba TPDC kuleta tawi lingine Kibaha na Bagamayo ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi kutumia gesi hii.

14. Tumehamasisha Mkampuni yote yaliyowekeza Mkoa wa Pwani kusajili TRA Pwani namba zao za utambulisho wa Mlipa kodi na kulipa kodi (TIN Number) zao ili kuongeza Mchango wa Mkoa katika Pato la Taifa.

15. Tumefanikiwa kutengeneza 20% ya ajira kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na 5% tu ya mwaka 2015/16.

16. Tumefanikiwa kutoa mchango wa Ajira 200,000 nchini kupitia viwanda hivi vilivyoongezeka ndani ya Mkoa wetu.

17. Tumehamasisha Ujenzi wa Viwanda Vikubwa 7 vipya kwa ajili ya kusindika mazao ya chakula na matunda (*Elven Agri Co. Ltd Kilichopo Mapinga - Bagamoyo, Sayona Fruit Processing Plant kilichopo Mboga Chalinze*), (*Bakhres Fruit & Processing Plant*) kilichopo Vikindu Mkuranga ambavyo vimejengwa mwaka 2017/2018. Viwanda vingine ni *Energy milling kilichopo Kibaha, Kuchi Jogoo Co. Ltd, Kiwanda cha kubangua korosho Terra Cashew kilichofufuliwa Juni 2018 na kiwanda cha CPL (T) Grain Processing and storage Co cha Unga.*

18. Tumehamasisha Ujenzi wa viwanda vikubwa vipya zaidi ya kumi (10) vya vifaa vya Ujenzi kama vile Nondo, Vigae, Saruji Matofali vyote vimejengwa katika kipindi hiki cha awamu ya Tano.

Makampuni hayo yaliyowekeza ni ***Kiluwa Steel Group - Mlandizi Kibaha, Hongyou Steel Co. Ltd - Zegereni Kibaha, Lake Steel and Allied Products Co. Ltd - Misugusugu Kibaha, Lodhia Steel Group - Kisemvule Mkuranga, Fujian hexiwang Industry Ltd- Kisemvule Mkuranga, kwa upande wa vigae ni Goodwill Ceramics - Mkiu Mkuranga, KEDA Ceramics - Chalinze, na Tofali ni Shafa Investmet Ltd.***

19. Tumehamasisha Ujenzi wa Viwanda Vikubwa vipya vitano (5) vya Kuunganisha Magari, mabasi, Trekta, na malori makampuni yaliyowekeza ni ***BM Motors Zegereni (Mabasi), GF Vehicle Assembly (malori), Nyumbu Project (Magari ya zimamoto) URUSUS Tractor Assembly Plant (Matrekta), Equtor Suma JKT (Magari ya zimamoto***).

20. Tumehamasisha Ujenzi wa Viwanda vikubwa vipya viwili (2) vya Madawa na vifaa tiba (Kairuki Pharmaceutical Ltd na Bahari Pharmacy).

21. Tumehamasisha Ujenzi wa Viwanda vikubwa viwili vya Sekta ya Mifugo na Machinjio ya Kisasa yaani TANCHOICE Ltd, Machinjio na kiwanda cha Chanjo za Mifugo Hester Bioscience.

22. Tumefanikiwa kuhamasisha ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kutengeneza Aluminium trailers kwa ajili ya kubebea mafuta. Kiwanda kimekamilika, kipo Kibaha Picha ya Ndege kinasubiri kuzinduliwa tu.

23. Tumehamasisha ujenzi wa Kiwanda cha Mitungi ya gesi (Lake gas) na tayari kimeanza kufanya kazi na kinatengeneza

Mitungi 60,000 kwa mwaka. Hiki ni kiwanda pekee Tanzania ambacho kitasaidia kuokoa misitu yetu isiteketee kwa kuni na mkaa.

24. Tumefanikiwa kuhamasisha ujenzi wa Viwanda vingine vikubwa vya kipekee ndani ya miaka hii mitano. Viwanda hivyo ni kama vile viwanda vya Gypsum, Nyaya za Umeme, Nyavu za Uvuvi, Mikate (Royal Supermarket Ltd), Kampuni ya KOM Group yenye Makao Makuu yake Kahama Shinyanga, Nyuzi, kuchakata Mihogo, kuchakata Samaki, Sabuni za unga, Dypers za watoto, Misumari, vifungashio, Vipodozi ikiwemo vitakasa mikono (Sanitizer), mabomba ya plastiki na vifaa vya plastiki.

25. Tumefanikiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kuwa Masoko ya malighafi na bidhaa nyingi za wakulima hupatikana ndani ya Mkoa na kuwezesha vijiji hivyo na Halmashauri kupata mapato yatokanayo na malighafi mfano; *Kaoline - Pugu, Dolomite - Msoga, Mchanga - Ruvu, Feldspar - Handeni, Bwani, Gairo na Soapstone - Dodoma, Mahindi - Miono, Mananasi Kiwangwa.*

26. Tumefanikiwa kuongeza mapato ya TRA Kutoka Sh. 64.9 bilioni Mwaka 2011-2015 hadi Sh. 147.2 Bilion mwaka 2016-2019.

27. Tumefanikiwa kuhamasisha Makampuni yote yaliyowekeza Mkoa wa Pwani kusajili namba zao za utambulisho wa Mlipa kodi TRA Mkoa wa Pwani na kulipa kodi zao ndani ya Mkoa wetu ili kuongeza Mchango wa Mkoa katika Pato la Taifa.

28. Serikali imekamilisha ujenzi wa Bandari ya Nyamisati uliogharimu kiasi cha shilingi bilioni 14.5 na kukamilika kwa meli

mpya iliyogharimu kiasi cha shilingi bilioni 5.5 itakayobeba Tani 100 za mizigo, abiria 200, na magari 6 kati ya Mafia na Nyamisati. Hatua hii ni muhimu katika kufungua fursa za biashara na uwekezaji Wilayani Mafia. Bidhaa za aina zote zitapungua bei kwa mlaji.

29. Jamii zetu zinazozunguka maeneo ya Viwanda na Uwekezaji zimepokea Michango mingi mbalimbali ya wadau wa viwanda kama Community Social Responsibility (CSR). Michango hiyo ni kama ujenzi wa madarasa, visima vya maji).

30. Ujenzi wa Soko la Halmashauri ya Mji Kibaha litakalogharimu Shilingi Bilion 2.2. Kazi ya ujenzi bado inaendelea. Hata hivyo, tayari kuna stendi mpya ya mabasi iliyogharimu Shilingi 3.2bn/- ambayo imechangamsha mji na biashara hapa Kibaha.

31. Tuliomba Mradi wa ujenzi wa Soko la Samaki Bagamoyo. Maombi yamepokelewa, fedha bado haijatolewa Shilingi Bilioni 1.6.

32. Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha iliomba ujenzi wa Soko la Kisasa Mlandizi. Maombi yamepokelewa, tunasubiri fedha kutoka Hazina shilingi Bilioni 7.7.

33. Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe tuliomba Mradi wa ujenzi wa Kiwanda cha Kubangua Korosho Shilingi Bilioni 2.8. Maombi yamepokelewa, pia fedha hizi bado hazijatolewa na Hazina.

34. Katika Maradi wa SGR Makampuni na Viwanda Mkoa wa Pwani wamenufaika kwa kutoa huduama na bidhaa za ujenzi. Baadhi ya Makampuni hayo ni Ako Group - Chakula, Arel Hotel - Malazi, Lake Steel - Nondo, Lodhia Steel Gulf Conrete - Kokoto.

35. Ujenzi wa viwanda umesababisha miji kukua na biashara ndogo na kubwa kuongezeka. Mahitaji ya nyumba za kupanga yameongezeka.

36. **AFYA:** Hospitali 3, Vituo vya Afya18, Zahanati, Madawa, Vifaa tiba. Hivyo vyote vimewezekana ili Mtu wa Pwani awe na Afya njema na ashiriki katika uchumi wa Pwani na Taifa kwa ujumla.

Katika Kipindi cha miaka mitano ijayo 2020-2025, pamoja na mambo mengine yaliyopo kwenye ilani ya 2020 kwa Mkoa wa Pwani Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi inakusudia kutekeleza miradi mbali mbali ya Kimkakati itakayolenga kuongeza ukusanyaji wa Mapato, Ajira, Ujenzi wa Viwanda na Kuboresha Huduma za Jamii.

Baadhi ya Miradi ni Pamoja na:-

a) Mradi wa Bagamoyo Sugar Limited; Mradi huu unatekelezwa na Bakhresa Group katika Kijiji cha Makurunge Wilayani Bagamoyo kwenye eneo la hekta 10,000 kwa ajili ya kilimo cha miwa na ujenzi wa kiwanda cha sukari. Kwa sasa mradi upo kwenye hatua mbalimbali za uendelezaji ikiwemo Ujenzi wa Kiwanda na kuendelea kandaa vitalu na kuandaa mashamba. Malengo ya uzalishaji wa sukari ni tani 35,000 kwa mwaka utaanza rasmi 2021. Pamoja na sukari, kampuni hiyo katika awamu ya pili

itajenga pia kiwanda cha kuzalisha ethanol kutokana na mabaki ya miwa. Awamu ya mwisho ni kuzalisha tani 100,000 za sukari na kutengeneza ajira 2000.

b) Mradi wa Stigler's Gorge - Huu ni mradi wa Kitaifa wa kuzalisha Umeme Megawati 2,115 za umeme katika maporomoko ya mto Rufiji katika mikoa ya Pwani na Morogoro. Kukamilika kwa mradi huu kutamaliza tatizo la umeme ambalo ni hitaji muhimu kwa ajili ya uzalishaji viwandani, itakuwa ni historia. Kwa hiyo utavutia uwekezaji zaidi. Manufaa mengine ya mradi huu ni kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, utalii na udhibiti wa mafuriko maeneo ya chini ya Mto Rufiji. Kwa sasa mradi upo katika hatua ya utekelezaji.

c) Mradi wa Bandari Kavu Kwala - Mradi huu upo Halmashauri ya Kibaha. Uwepo wa Bandari hii kavu inamaanisha magari makubwa ya mizigo kutoka mikoa ya bara yataishia eneo la Kwala, hali itakayochochea maendeleo ya sekta nyingine za uwekezaji ikiwemo sekta ya viwanda na huduma. Kwa sasa mradi umekamilika na tulipokea Makasha ya kwanza ya Makontena kutoka Dar es Salaam Aprili 2020.

d) Ujenzi wa Reli ya Mwendokasi ya Stiglers Gauge: Mradi huu ni wa Kitaifa. Kwa Mkoa wa Pwani kutakuwa na vituo 3 vya Soga, Ruvu na Kwala na kituo cha Ruvu kutakuwa na chumba cha barafu cha kuhifadhia mbogamboga ambayo ni fursa kwa Wakulima Ruvu wanaolima katika Bonde la Mto Ruvu.

e) Ujenzi wa Daraja jipya la Wami litakalo gharimu 67.779 Bilioni litakalo punguza kwa kiwango kikubwa ajali kwenye eneo hilo na kuunganisha vizuri Mkoa wetu na Mikoa ya Kaskazini.

f) Kujenga vyuo vipya viwili vya VETA Wilayani Mafia - Ndagoni na Kingine Wilayani Rufiji - Utete ambavyo vitawezesha vijana kupata ujuzi mbalimbali kwa kujiajiri na kuajiriwa viwandani.

g) Serikali imepanga kuanzisha Wilaya Mpya ya Chalinze Ili kusogeza huduma kwa wananchi.

h) Serikali inakusudia pia kupanua barabara ya Kibaha - Chalinze kwa Njia nane (zaidi ya Kilometa 70).

i) Tutaendelea kushirikiana na Sekta binafsi kuandaa maonesho ya Viwanda na Biashara na Maonesho ya Sekta ya Utalii Kimkoa kila Mwaka ili kukuza biashara hizo, (Maonesho ya Utalii katika Wilaya yetu ya Mafia).

j) Tunaendelea kufanya ufuatiliaji baada ya Mwekezaji kuwekeza ndani ya Mkoa wetu (after care services) ili kuhakikisha anaendelea na uwekezaji bila kupata vikwazo vyovyote.

Ndugu Washiriki,

<u>Changamoto</u>

Katika kipindi cha miaka mitano 2015-2020 zipo baadhi ya changamoto zilizokumba sekta ya viwanda, Biashara na Uwekezaji , nazo ni kama zifuatazo:

a) Kukosa soko kwa bidhaa nyingi zinazozalishwa kwa viwanda vyetu hapa Mkoani Pwani, mfano, marumaru (tiles), nondo, saruji, *PVC Pipes* mabomba ya maji, *conduits pipes*, *square pipes*, *juice.* Hii

inatokana na bidhaa kama hizi zinaagizwa kutoka nje ya nchi kwa kodi nafuu na kupelekea bidhaa za ndani kukosa soko. Bidhaa zinazozalishwa zikipata soko la ndani ya nchi tutalinda viwanda vyetu lakini pia tutakuwa tunalinda ajira za wananchi wetu.

b) Ajira kwa wananchi wa Pwani bado ni kidogo sana ambazo ni takribani 20% hii ni kutokana na vijana wanaotakiwa katika ajira hizo ni wale wenye utaalamu wa fani mbalimbali ambao ni wachache. Ni jukumu la wananchi wa Mkoa wa Pwani kukazania elimu, hususan kwenye vyuo vya VETA vinavyojengwa Mkoani kwetu.

c) Umeme: Mahitaji ya umeme ni MW 73 na unaopatikana ni MW 50 hivyo tunaupungufu wa MW 12.

d) Maji: Maeneo mengi yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda hayana maji ya uhakika, hii ni changamoto kubwa kwa DAWASA.

e) Upatikanaji wa nishati ya Gesi viwandani; wawekezaji wengi wanahitaji kutumia gesi lakini changamoto ni kuwa bomba la gesi limepita mbali. Tunahitaji tuwe na tawi kuja Kibaha na Bagamoyo.

f) Upatikanaji wa vibali vya kazi na makazi kwa wafanyakazi wa Kigeni. Idara ya Kazi inafanyia kazi changamoto hii.

g) Baadhi ya viwanda kutozingatia Sheria za Mahusiano kazini kwa kulipa wafanyakazi mishahara midogo, kufukuza pasipo kufuata sheria na kuajiri bila mikataba, kutowapatia vitendea kazi, kuwatelekeza wanapoumia kazini, kutowakatia BIMA ya Afya, kutowapatia likizo, kutowapa posho zinazostahili, n.k.

Ndugu Washiriki, baada ya Mafanikio haya niliyoyaeleza;

Sote tumeshuhudia **PWANI ya mwaka 2015 siyo PWANI ya mwaka 2020.** Tunafahamu faida ya kuwa na Viwanda na kukua kwa biashara katika Mkoa wetu na Nchi kwa ujumla. Faida hizo ni pamoja na:

- Upatikanaji wa Malighafi za ujenzi wa Nyumba za Makazi, Miundo mbinu za Barabara na Reli kwa bei nafuu. Serikali inaokoa pesa nyingi za Kigeni kwa kuto kuagiza vifaa hivi nje ya nchi, Mfano; ni Ujenzi wa Mradi wa Standard Gauge asilimia kubwa ya malighafi zake zinatoka hapa nchini, Inatoa ajira, Ulipaji wa Kodi kwa Serikali Kuu, Ulipaji wa Ushuru wa Huduma (Service Levy).
- Viwanda hivi vinaongeza ujuzi kwa nguvu kazi “Skills Development”.
- Viwanda hivi ni vichocheo vya ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi na huduma mfano; Kwenye Taasisi za Mafunzo (VETA), Uchimbaji madini, Usafirishaji, Kwa faida hizi **itoshe kusema kupitia uwekezaji wa viwanda tumeweza kupambana na Umaskini.**

Ndugu Washiriki;

Nimalizie kwa kuwashukuru kwa kuitikia wito wa kushiriki kikao hiki japo taarifa zilikuwa za muda mfupi. Niwaombe tushiriki kikamilifu katika kuwasilisha taarifa fupi za mafanikio ya miaka mitano kutoka sekta zenu na kutoa mapendekezo kwa Serikali.

Asanteni kwa kunisikiliza.